

# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA**

Tel: +255 25-2802163

Fax: +255 25 2802163

E-mail:[md.sumbawanga@rukwa.go.tz](mailto:md.sumbawanga@rukwa.go.tz)



P.O. Box 187

**SUMBAWANGA**

19/05/2018

## **TANGAZO LA ZABUNI.**

### **NAMBA YA ZABUNI: LGA/098/2017-2018/NC/01**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Sumbawanga anawatangazia kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 anatarajia kutumia Wakala wa kukusanya Ushuru kwenye chanzo cha Mapato kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini.

| NA | JINA LA ZABUNI  | ZABUNI NAMBA            | ENEO                    |
|----|-----------------|-------------------------|-------------------------|
| 1  | USHURU WA MAZAO | LGA/098/2018-2019/NC/01 | MANISPAA YA SUMBAWANGA. |

#### **MASHARTI YA MUOMBAJI.**

1. Muombaji lazima awe na Leseni ya biashara, TIN, hati ya usajiri na ofisi inavyoonekana na kutambulika.
2. Muombaji awe na uwezo wa kifedha ,athibitishe kwa kuambatanisha bank statement ya miezi mitatu iliyopita kutoka tarehe aliyoomba .
3. Yeyote anayeomba Zabuni kwa niaba ya kampuni ,atatakiwa kuwasilisha POWER OF ATTORNEY iliyothibitishwa na Mwanasheria.
4. Dhamana itakuwa fedha taslimu ya miezi mitatu ya kiwango utakachotenda kwa Mzabuni atakayeshinda.
5. Muombaji awe tayari kutumia viwango vilivyowekwa na sheria ndogo za Halmashauri na sheria nyingine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
6. Mashine zitakazotumika kukusanya ushuru zitatolewa na Halmashauri.
7. Muombaji atawasilisha makusanyo yote Manispaa ,pia atatakiwa kuonyesha kwamba yupo tayari kulipwa asilimia ngapi ya makusanyo.
8. Muombaji anatakiwa kulipa ada ya Zabuni kiasi cha Tsh 50,000/= ambayo haitarudishwa.

9.Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatanisho husika (**company profile**) nakala halisi ya maombi iambatane na nakala kivuli moja, weka katika bahasha funga kwa lakiri tuma kwa:\_

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MANISPAA,

S.L.P 187,

**SUMBAWANGA.**

Maombi yatapokelewa ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni ghorofa ya tatu chumba namba sita.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 1/06/2018 siku ya Jumanne saa 4.00 Asubuhi** na ufunguzi utafanyika muda huo huo katika ukumbi mkubwa wa Manispaa.

Limetolewa na:



MKURUGENZI WA MANISPAA  
SUMBAWANGA.  
